

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO  
(MAENDELEO YAJAMII)**



**TAARIFA KWA UMMA**

Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali anayakumbusha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini kuwasilisha Taarifa za Mwaka kwa mujibu wa Kifungu Na. 29 cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 24 ya mwaka 2002 na Kanuni Na. 10 ya Kanuni za Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2004 (GN 152, 2004) kama ilivyorekebisha na Kanuni Na. 6 ya Kanuni za Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2014 (GN 8, 2015), kabla ya tarehe 15 Aprili, 2018. Taarifa hiyo ijumuishe Taarifa za utendaji kazi, Taarifa za fedha zilizokaguliwa, NGO Fomu Na.10 na Stakabadhi ya malipo ya ada ya mwaka. Mashirika yatakayoshindwa kutekeleza agizo hili ndani ya kipindi tajwa, yatachukuliwa hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kutozwa faini.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'M.S. Katemba', written over a horizontal line.

M.S. Katemba  
**MSAJILI WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI**